TOLEO NO.67

# Khilafah

RABI THANI 1447 HIJIRIA — OKTOBA 2025 MILADIA ( Bei Tsh 4,000/= - Ksh 200/=)

NDIO SULUHISHO

## UCHAGUZI WA KIDEMOKRASIA NI MINONG'ONO YA IBILISI



**Habari:**

Mnamo 13 Septemba 2025 kinyang’anyiro cha kuwania urais wa Zanzibar kilianza rasmi huku chama tawala – Chama Cha Mapinduzi (CCM) na chama cha upinzani cha ACT-Wazalendo kikizindua kampeni zao. CCM ilisisitiza ‘utulivu’, ‘amani’ na ‘umoja’, huku chama cha ACT Wazalendo kikiweka kipaumbele katika uwajibikaji, usawa, na fursa za kiuchumi.

**Maoni:**

Kwa sasa, Tanzania iko kwenye kipindi cha kampeni za uchaguzi hadi 28 Oktoba 2025 ambapo tarehe 27 Oktoba 2025 itakuwa siku ya kupiga kura kwa ajili ya uchaguzi wa Zanzibar, huku Jumatano 29 Oktoba 2025 itakuwa siku ya kupiga kura kwa Jamhuri ya Muungano kwa mujibu wa Tume Huru ya Uchaguzi ya Tanzania.


Huu ni uchaguzi wa tano wa vyama vingi tangu Tanzania ilipoamua kutabanni demokrasia ya vyama vingi vya kisiasa mwaka 1992. Uchaguzi wa mwaka huu ulionekana kuwa na matukio sawa na yale ya awali, kuna hali ya kutojali, kukabiliwa na kususiwa, kuwepo kwa

**Inaendelea Uk. 3**

## Yaliyomo :


- **Wazee sio nakama bali ni Baraka ..........................................2**
- **Siku ya afya ya akili duniani ..........................................4**
- **Maangamizi ya Gaza ni maangamizi yetu Umma wa Kiislamu .......7**


## KUTAMBULIWA KWA DOLA YA PALESTINA KUTAMBULIWA KWA MAYAHUDI KUNYAKUA 78% YA PALESTINA!



Uingereza, Canada, Australia na Ureno zililitambua ile inayoitwa “Dola ya Palestina,” na kufuatiwa na nchi kadhaa katika mkutano wa ngazi ya juu wa kimataifa wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa uliofanyika kuanzia Septemba 22-30, 2025, na ulioongozwa na Ufaransa na Saudi Arabia. Utambuzi huu ulikaribishwa na watawala Ruwaibidha (wajinga wasio na maana) wa Waislamu, pamoja na Jumuiya ya Ushirikiano wa Kiislamu na Jumuiya ya Waarabu. Jambo la kushangaza ni kwamba, ilikaribishwa pia na mashirika ya Kipalestina, ambayo yanaona kuwa ni matunda ya uthabiti wao, kana kwamba Palestina imekombolewa na na umbile la Kiyahudi kung'olewa!

**Enyi Waislamu:** Moja ya mahitaji muhimu ya ufahamu wa kisiasa ni kuifanya itikadi ya Kiislamu kuwa msingi wakati wa kuhukumu mambo na vitendo. Haijuzu kwa Muislamu kutoa hukumu juu ya

**Inaendelea Uk. 6**

## WAZEE SIO NAKAMA BALI NI BARAKA

Tarehe 1 Oktoba ni Siku maalumu Kimataifa ya Wazee. Mnamo mwezi Disemba 1990, Umoja wa Mataifa ulipiga kura kuichagua siku hiyo kwa mujibu wa Azimio 45/106. Na ikaanza rasmi kuadhimishwa siku hiyo mwezi Oktoba wa mwaka uliofuatia 1991.

Siku hiyo huadhimishwa kila mwaka ili kutambua nafasi ya wazee katika maisha na kuangazia changamoto mbalimbali zinazowasibu. Aidha, siku hiyo huwa ni fursa ya kutambua mchango, busara na maarifa ya wazee kwa maendeleo na kutoa msisitizo wa kuongezwa juhudi ya kuangalia ustawi wao.

Uzee ni dalili ya uwepo wa Muumba Anayesarifu mambo yote yakiwemo maumbile ya mwanadamu na kumpangia mwanadamu atakavyo bila ya matakwa yake. Kwa kuwa hakuna mwanadamu anayechagua kuwa awe mzee lakini kila umri ukiongezeka mwanadamu hubadilika na mwisho kuwa mzee. (Surat Insan :28)

Aidha, uzee ni kielelezo cha udhaifu wa mwanadamu kwa sifa yake kama kiumbe, kwa kuwa kila kiumbe kwa maumbile yake kina udhaifu na kina mipaka. (Surat Maryam: 4)

Bali uzee ni muda wa kukosa nishati baada ya nguvu. Kwa hivyo, kimaumbile mwanadamu kama alivyokuwa mchanga na mdogo kipindi cha uzee pia huwa ni muhitaji zaidi wa msaada kuliko wakati mwingine. Ni kipindi ambacho akili na kiwiwili huwa vimedhoofika nguvu. (Surat Ar-rum: 54)

Uzee katika ubepari ni nakama kwa sababu kwa kipimo chao cha 'maslahi' mzee hazalishi kwa kuwa hana nguvu ya kufanya kazi. Na ubepari una msemo usemao 'asiyefanya kazi asile. Kwa msingi huo kwa mujibu wa mfumo wao batil mzee anaongeza umaskini na ni mzigo unaohitaji kulishwa, kuvishwa, kutibiwa nk. bila ya kuingiza chochote katika kuzalisha.

Aidha,kwa kipimo cha ubepari cha fikra za za 'uhuru binafsi' mzee anakuwa kizuizi kwa familia kupata muda na faragha ya kustarehe. Kwa hivyo, kwao mzee ni kero na shida inayozuiya watu kujifaragua na uhuru wao wa kustarehe na kula maraha ya maisha.

Kwa hivyo, ndio maana nchi za kibepari wana suluhisho la kuwarundika na kuwatupa katika majumba ya wazee. Jambo ambalo ni khiyana na uovu mkubwa anaofanyiwa wazee baada ya kuwalea watoto wao kwa dhiki na tabu na baada ya kuchangia maendeleo ya ustawi wa nchi yake.

Uislamu umewajibisha watoto kuwatunza wazazi wao. Hilo ni katika ibada kubwa. Na ni katika laana na madhambi makubwa kuwatupa wazazi hususan wakiwa wazee hata kama ni makafiri. Aidha, chini ya Khilafah qadhi ana mamlaka ya kuingilia kati jambo hili kwa kutolewa kwa nguvu sehemu ya mapato ya mtoto kwa ajili ya kuwahudumia wazazi wake. Na kama watoto hawana uwezo huangaliwa wanaofuatia katika jukumu la kisharia. (Surat Bani Israil: 23-25)
Aidha, Uislamu umehimiza ndoa na ukahimiza mke awe mwenye uzazi na mchamungu ikiwa pia ni suluhisho la kuwatunza wazazi katika uzee wao

Pia ni wajibu jamii kwa ujumla kuamiliana na wazee kwa wema kama na umewapa hadhi maalumu/ tunzo maalumu hata kama ni makafiri (Dhimiy) nk.
Hadhi hizo ni kama kupewa heshima, Mtume SAAW anasema:
'Sio katika Sisi asiyewarehemu wadogo zetu na kuwaheshimu wakubwa (wazee) wetu'
Wazee makafiri hawalipi jizya, hawapigwi katika jihadi, na kama mzee hana wa kumuhudumia ni wajibu wa dola (Khilafah) kumuhudumia, awe alikuwa muajiriwa rasmi au mtu wa kawaida tu.

Mhariri

**01 Rabiul Awwal 1447 Hijria**

**Septemba 2025 M**

***jukwalakhilafah@gmail.com***

## Uchaguzi wa kidemokrasia .. *Kutoka uk .1*

hisia za mashaka kwamba hautakuwa uchaguzi huru na wa haki, kwani mchakato wa mageuzi ya uchaguzi haujafanyika.
Suala la demokrasia na kila kitu kinachohusiana nayo, kama vile kushiriki, kuunga mkono kampeni za kidemokrasia na uchaguzi wake liko wazi kwa mujibu wa Uislamu.

Hukmu ya Kiislamu juu ya kupiga kura kwa mfumo usiokuwa wa Kiislamu imeharamishwa (haram) na pia hairuhusiwi kuutekeleza au kuulingania. Katika mtazamo mpana zaidi katika Uislamu hairuhusiwi kutekeleza, kushiriki, kutabanni au kulingania mfumo wowote ulio kinyume na Uislamu.

Suala la sheria na hukmu katika Uislamu haliwezi kuchukuliwa kutoka kwa mfumo uliotunga na mwanadamu, kama vile demokrasia ambayo ni mfumo wa kisiasa wa kibepari. Ni lazima itoke kwa Mwenyezi Mungu (swt) pekee. Kwa hivyo, mfumo wowote wa kisiasa, kijamii au kiuchumi ambao haujaegemezwa kwenye Sharia ya Kiislamu hauna nafasi katika Uislamu na lazima ukataliwe.

Kiuhalisia, umma kwa jumla iwe Zanzibar, Tanzania, Afrika na duniani kwa jumla wanajua kabisa kuwa demokrasia imewafelisha. Zaidi ya hayo, hakuna tofauti kati ya chama tawala na upinzani, kwa vile vyama vyote vya kisiasa vya kidemokrasia vinashikilia msingi ule ule wa itikadi ya kibepari ya kisekula, ya kikoloni ya maslahi ya kibinafsi, unyonyaji na kutenganisha dini na maisha ya watu.
Nchi nyingi za Kiafrika isipokuwa chache sana kama Tanzania sasa zinatawaliwa na vyama vilivyowahi kuitwa vya upinzani, lakini hakuna kilichopatikana katika nchi hizo. Bado, Afrika ndilo bara lenye umaskini zaidi licha ya kuwa na maliasili nyingi ambazo kupitia ukoloni mamboleo wakoloni wa Magharibi wanazinyakua bure kupitia wanasiasa tunaowachagua kila uchao chini ya demokrasia!

Afrika na dunia hazihitaji uchaguzi wa kisekula wa udanganyifu ambao hufanya kazi tu kwa ajenda ya kikoloni ya kinyonyaji bila kuleta mwamko wowote wa kweli kwa watu.

Mfumo badali pekee na nidhamu badali ya kisiasa lazima zitokamane na Uislamu na nidhamu ya kisiasa ya Kiislamu mtawalia. Chini ya Uislamu ambao ni mfumo wa Mwenyezi Mungu kutoka kwa Muumba wa ulimwengu nidhamu ya kisiasa ya Kiislamu ya haki na uadilifu chini ya uongozi wake wa kisiasa wa kimataifa wa Khilafah ungewekwa barani Afrika.

Katika hatua hiyo Afrika na dunia itakuwa huru kutoka katika minyororo ya maovu na mfumo wa kidemokrasia wa kinyonyaji, pia itashuhudia uongozi halisi na wa kweli na maendeleo ya haraka, tofauti na uharibifu, kurudi nyuma, umaskini uliokithiri, unyonyaji ambao ulileta na uvamizi wa mkoloni mwishoni mwa karne ya 19 CE hadi sasa.

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

*******

## MATUKIO YA TARIIKH MWEZI WA RABI-UL THANI

**1.Vita vya Bahrain**

**Mtume Saaw aliongoza doria kubwa ya kiasi cha kikosi cha askari 300 katika mji wa Bahrain. Hakukutokea mapigano yoyote. (Mwaka wa 3AH.)**

**2.Kutumwa kikosi cha Abuu Ubeida Ibn Jarrah**

Mtume SAAW alituma kikosi hiki cha watu 40 kuelekea Dhi al-Qiswa kwa Bani Thaalabah, baada ya kuuwawa wenzake Muhammad bin Maslamah. Maadui wakashambuliwa na kushindwa. (Mwaka wa 6 AH)

**3. Kutumwa kikosi cha Zaid bin Harithah**

Kilitumwa katika mji wa Al Jumumu kwa Bani Saleem. Kwa msaada wa mwanamke wa Bani Muzaina Waislamu waliweza kushinda kiurahisi (6AH)

4.Jemadari mkubwa wa Kiislamu Khalid bin al-Walid afariki dunia Mwaka 21 Hijria

**5. Kuanza Vita vya Jamal ndogo**
(25 Rabiu-al Thani- Mwaka wa 36 AH.)

6. Kujiuzulu Uongozi kwa Khalifa wa tatu wa Bani Umayya Mu'awiya bin Yazid (Muawiyah II) Mwaka 64 Hijria (Disemba 21, 683 miladi)

7. Kifo cha Khalifah wa kumi wa Bani Umayyah, Hisham bin Abd al-Malik bin Marwan ndani ya Syria mwaka 125 Hijria – (Februari 6, 743 miladi)

*****


# SIKU YA AFYA YA AKILI DUNIANI

Kila tarehe 10 Oktoba ya mwaka huadhimishwa kuwa ni Siku ya Afya ya Akili kimataifa. Lengo lake likiwa ni kuelimisha jamii kuhusu afya ya akili, changamoto zake na ni jinsi gani ya kutunza afya hiyo.

Afya ya akili ni ile hali ya ubongo kufasiri kwa usahihi taarifa zinazoakisiwa kwake kupitia milango ya fahamu, yaani uwezo wa kuvitambua vitu kwa usahihi wake.

Changamoto ya afya ya akili ni pale ubongo unapofasiri vitu kimakosa (delusion) au kufasiri vitu ambavyo havipo wala kiuhalisia havijadirikiwa na milango ya fahamu (hallucinations). Mathalan, mtu kusikia sauti zisizokuwepo katika uhalisia (auditory hallucinations) ima iwe watu wanamzungumzisha (2nd person hallucination) au watu wanazungumza wao ila yeye anawasikia (3rd person hallucination), kuhisi harufu zisizokuwepo (olfactory hallucination/phantosmia), au kuona visivyokuwepo (visual hallucination). Yote haya ni changamoto kwenye ubongo, ambapo hupelekea kufasiri vitu visvyo kuwepo

Changamoto kubwa ya afya ya akili ambayo ipo katika jamii zetu ni sonona (depression). Ugonjwa unaosababishwa na msongo mkubwa wa mawazo ya muda mrefu, ambao baadae huathiri ubongo na kupelekea mtu kubadilika tabia ikiwemo kujitenga na watu, na baadae kuanza kupata mawazo ya kukatisha uhai au kusikia watu wakimlazimisha akatishe uhai wake.




Changamoto hiyo ndio inayoongoza katika wodi au clinic za wagonjwa wasio na afya ya akili. Taasisi ya Kitaifa ya Masuala ya Afya ya Akili nchini Marekani (NIH) katika ripoti yake ya mwaka 2023 inaonesha kuwa asilimia 5 hadi 17 ya watu duniani wana tatizo la sonona, na wastani wake ni asilimia 12. Huku wengi wao wakiwa wanawake kuliko wanaume.

Pia jarida la Forbes Health linaonesha asilimia 5 ya watu dunia wenye umri kuanzia miaka 18 wana sonona. Sonona ndio ugonjwa ambao hupelekea watu wengi kuwa na mawazo ya kukatisha uhai wao hasa vijana.

Shirika la Afya Duniani (WHO) linaonesha kuwa sonona (depression) ndio ugonjwa wa akili namba moja duniani, na ndio sababu namba moja ya kujitoa uhai kwa wenye umri kati ya miaka 15 hadi 29, ambapo kila baada ya sekunde 40 duniani kuna mtu mmoja anakatisha uhai wake, ilhali Tanzania watu 3000 walikatisha uhai wao kwa mwaka 2016, na ikiwa ni nchi ya nne Afrika kwa watu wake kukatisha uhai wao.

Sababu kadhaa huchangaia kuathiri afya ya akili hususan sonona kama hali duni ya kiuchumi, sababu za kijamii, kutojithamini (low self-esteem) nk.

**1. Sababu za kiuchumi;**

Hali mbaya ya kiuchumi imepelekea watu wengi katika jamii zetu kukata tamaa ya maisha, wengine wakikumbwa na msongo wa mawazo na hatimae kupata sonona. Asilimia kubwa ya watu katika ulimwengu wa leo chini ya ubepari hawafikii mahitaji yao ya kimsingi. Na hii hupelekea wengine kukimbia familia na hatimae mama aliyeachiwa familia kufanya maamuzi yasiyo yakawaida kama ilivyotokea Geita mama aliyewapa watoto wake wanne sumu na yeye mwenyewe kunusurika kifo kwa kunywa sumu baada ya kuwahishwa hospital. Kipi kinachofanya mtu kuwa na maamuzi magumu kiasi hata cha kukatisha uhai wake na watoto, si kingine bali itabainika kuwa wengi wao hukumbwa na sonona yenye kuleta mawazo hayo ya kukatisha uhai (suicidal ideation), kabla ya kutekeleza maamuzi hayo.

**2. Sababu za Kijamii:**

Hapa tutazungumzia hasa zile za kimapenzi. Hii ndio sababu kubwa ya msongo wa mawazo na kukatisha uhai kwa vijana kati ya umri wa miaka 15 hadi 29. Daktari Praxeda Swai ambae ni mganga mkuu wa kitengo cha matibabu ya wagonjwa wa akili katika hospitali ya taifa Muhimbili anasema kuwa "maranyingi watu hukatisha uhai wao kwa kushindwa kutatua matatizo ya kihisia yanayowakumba".

**Inaendelea uk ..6**

Mfano tukio liliotokea sinza-Dar es salaam mwishoni mwa mwezi Julai 2021 ambapo kijana wa miaka 29 aitwae Alex Korosso alimuua mwenzie na kisha yeye mwenywe kujipiga risasi wakiwa Bar baada ya kugombea kinywaji, lakini uchunguzi ulionesha kuwa alikua na changamoto kwenye mahusiano yake ya kimapenzi kwa muda mrefu. Hivyo, utaona ni jinsi gani mahusiano mabovu ya kimapenzi (toxic relationships) yanavyowatesa vijana hasa ambao ni wanaanza kupata uzoefu wa kimaisha. Aidha, baadhi baada ya kufanyiwa vitendo vya kikatili, na hii hasa kwa wasichana ambao hufanyiwa vitendo vya ubakaji wengi wao wamekua wakikumbwa na changamoto ya afya ya akili ijulikanayo kama "post-traumatic Stress Disorder" na depression na baadhi yao hukatisha uhai kwa kushindwa kuishi na fedheha hiyo. Mfano katika utafiti uliofanywa katika majimbo kadhaa ya Marekani na Shirika la Center of Disease Control (CDC) imeonesha kuwa asilimia 27 ya wsichana wamefanyiwa vitendo vya ukatili wa kingono na asilimia 44 hawajihisi kuwa salama wanapotembea barabarani. Hili likaongeza idadi ya vijana wengi ambao wanachangamoto ya akili sonona na PTSD. Pia kuna sababu nyingine nyingi kama matumizi ya pombe yaliyopitiliza, matumizi ya dawa za kulevya na bangi nk.

**3. Hali ya Kutojithamini (low self-esteem).**

Hali hii mara nyingi imebebwa na mtazamo wa mtu juu kitu au jambo fulani. Kwa mfano, kuna wanaoona hana thamani kwa sababu hawana pesa. Wengine hujiona hawana thamani kwa sababu hawana elimu, cheo, nguvu au kutosikilizwa kile anachokihitaji. Hali hii ikidumu kwa muda hupelekea mtu kupata changamoto ya afya ya akili.

Mathalan, mnamo tarehe 27/06/2023 mtoto wa kike Zamda Jaffar (13) wa wilayani Kondoa mkoani Dodoma alijinyonga baada ya kutonunuliwa nguo ya sikukuu. Pia tarehe 05/06/2023 mwanafunzi Jaffar Mwashitete (16) wa kidato cha tatu wilayani Mbozi, Songwe alijinyonga baada ya kuhamishwa shule, kitu ambacho hakikumfurahisha. Pia mwanaume John Rugala (45) wa nchini Kenya alijiua baada kukasirishwa na kitendo cha mke wake kutompikia kuku tarehe 05/07/2023. Yote haya tukiyapima katika akili ya kawaida utaona si jambo rahisi mtu kukatisha uhai wake kwa sababu tajwa, bali haya ni mambo ambayo yamejikusanya kwa muda mrefu.

Adha, kuna wengine hujiona hawana thamani kwa sababu ya muonekano wao. Mfano, mtoto wa kike baada ya kuona wanaume wengi wa jamii yake wanapenda mabinti wembamba, basi nae atafanya jitihada za kujikondesha ili apendwe na watu wa jamii yake. Ndani ya Marekani na nchi za Ulaya mabinti wengi wameathiriwa na hili hii ambayo hatimae hujikuta katika ugonjwa ujulikanao kwa jina la "Anorexia nervosae" ambao ni upungufu ya lishe kwa khofu kuu ya kuongeza uzito na kujilazimisha mara kwa mara kudumisha uzito wa chini wa mwili, na pia hupatikana dhihirisho la ugonjwa kama 'marasmus' ambao ni upungufu wa lishe. Hali hiyo pia huwasibu wanawake wengi ambao hupendelea umbo la aina fulani, mpaka wengine hufanya upasuaji, hutumia dawa au hata kwenda mazoezi ili kupata maumbo hayo.

Sonona za aina hiyo hutibiwa na kitengo maalumu cha wanasaikolojia au madaktari wa magonjwa ya akili.

Hayo ni baadhi ya mambo ambayo asili ndio msingi wa changamoto ya afya ya akili katika ulimwengu wa leo. Na tunaona yote hayo ni mambo yenye kuepukika lakini fikra, nidhamu na sera za mfumo wa kibepari unaotawala dunia le ndio inatengeza mitazamo mibovu kwa watu wake na kupelekea sonona na changamoto nyingine za afya ya akili kukithiri ulimwenguni.

Uislamu chini ya nidhamu zake na fikra zake ni tatuo msingi la changamoto ya afya ya akili. Kwa mfano, katika upande wa kiuchumi Uislamu una nidhamu ya uadilifu ya kumfikia kila mtu juu ya mahitajio yake. Aidha, umepanga utaratibu mzuri katika matumizi ya mali za Umma ili kuwahudumia raia wote. Bila ya kusahau uwepo misaada ya kisharia kama Zakat ambayo husaidia mgawanyo wa rasilmali kwa watu nk.

Kwa upande wa nidhamu ya kijamii Uislam umepangilia mtangamano kati ya

**Inaendelea uk 6**

Kutambuliwa kwa dola ya Palestina ... *kutoka uk .1*

jambo au kitendo ambacho kiko mbali na itikadi ya Kiislamu. Kanuni ya msingi ni kuwa Muislamu asisahau kuwa suluhisho la dola mbili maana yake ni utambuzi wa umbile la Kiyahudi na kwamba lina haki kwa ardhi iliyobarikiwa, na jambo hilo limeharamishwa katika Shariah, kwani ni ardhi ambayo maswahaba watukufu waliinywesha kwa damu yao safi, pamoja na mujahidina waliowafuata kwa uadilifu. Ina msikiti wa tatu kati ya misikiti miwili mitakatifu, ambayo Waislamu husafiri kutoka sehemu zote za dunia kuiendea, na ni mahali pa Safari ya Usiku ya Mtume (saw). Palestina ni ardhi ya Kiislamu, na haijuzu kwa Muislamu kuiacha hata shubiri moja.

**Enyi Waislamu:** Je, mnatarajia mkuu wa ukafiri, Uingereza, na nchi nyingine za makafiri - zilizoitambua ile inayoitwa Dola ya Palestina - kutuma majeshi kuikomboa Palestina?! Uingereza ndiyo iliyoivunja Khilafah, ikatoa Azimio la Balfour, ikaweka Palestina chini ya Mamlaka, ikawezesha uhamiaji wa Mayahudi kutoka nchi mbalimbali za dunia kwenda humo, ikaweka dola kwa ajili ya Mayahudi huko, ikagawanya ardhi za Waislamu na kupandikiza watawala vibaraka juu yao ambao kazi yao kuu ilikuwa ni kulinda na kumakinisha umbile la Kiyahudi, na nyengine ni kudumisha kugawanyika kwa ardhi za Waislamu. Ama nchi zengine za kikafiri zilizoitambua Dola ya Palestina, zinalitambua umbile la Kiyahudi kwa 78% juu ya yake, ikiwemo kuisambazia mahitaji na mashini ya kijeshi ambayo kwayo inawauwa Waislamu huko Gaza, Ukingo wa Magharibi na kwengineko.

Je, mnatarajia umbile la Kiyahudi litakupeni fadhila kwa kuruhusu kuanzishwa kwa dola ya Palestina kwenye sehemu ya ardhi ya Palestina? Je, hamjui kwamba suluhisho la dola mbili, likipatikana, litakuwa ni kijidola dhaifu, kisicho na nguvu za kijeshi sawa na Mamlaka ya Palestina iliyopo hivi leo, ambayo si chochote zaidi ya kitengo cha usalama cha umbile la Kiyahudi, au eneo tu linalojitawala kwa maelekezo ya dola zilizotajwa na Biden? Na kwamba nchi kadhaa duniani hazina majeshi binafsi. Je, mutakubali kwamba matokeo ya mihanga yenu na uthabiti wenu yawe ni mamlaka ya uchungaji chini ya mishale ya Mayahudi?!

Kejeli hii inatukumbusha kejeli ya tamko la Yasser Arafat la kuanzishwa kwa Dola ya Palestina mnamo tarehe 15 Novemba 1988, nchini Algeria. Ilikuwa dola kwenye karatasi, lakini matunda ghafi ya mazungumzo ya Oslo yalikuwa mamlaka ndogo chini ya mishale ya Mayahudi.

**Enyi Waislamu:** Msisahau tunachowakumbusheni kila mara: suluhisho pekee sahihi na halali kwa kadhia ya Palestina ni kuhamasishwa kwa majeshi ya Waislamu ili kuikomboa Palestina yote na kuliondoa umbile la Kiyahudi kutoka uwepo.

Hizb ut Tahrir, kiongozi asiyewadanganya watu wake, mbebaji wa mradi mtukufu wa Khilafah, inakuombeni mufanye kazi nayo na inatoa wito kwa majeshi ya Waislamu yainusuru katika kusimamisha Khilafah Rashida ya pili kwa njia ya Utume. Ndani yake imo izza yenu na ndani yake liko suluhisho la matatizo yenu yote.

**Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

**Siku ya afya… kutoka uk 5**

mwanaume na mwanamke kibiashara kwa namna ya heshima na murua, na ukapangilia mahusiano mema ya mwanaume na mwanamke katika ndoa tu katika kuendea na kushibisha ghariza/ hisia ya kuendeleza kizazi na ukaharamisha zinaa na kuweka adhabu kali kwa mwenye kwenda kinyume. Hii maana yake ni kuwa hayo mahusiano yanayoitwa mahusiano hatarishi "toxic relationship" ambayo yanayopelekea vijana kati ya umri wa miaka 15 hadi 29 kuchanganyikiwa, kuleta sonono hadi kukatisha uhai wao hayatokuwepo tena.

Amma suala la mtu kujiona duni hana thamani hapa duniani. Kwa bahati mbaya katika ubepari thamani ya mwanadamu kwa kiwango cha elimu yake, cheo chake, hadhi yake, muonekano wake, kipato chake nk. lakini fikra ya Kiislamu inatuonesha kuwa mwenye thamani zaidi/ mbora wa watu ni mchamungu wao. Kama anavyosema Allah (s.w) katika Qur'an Tukufu:

"Enyi watu, hakika tumekuumbeni kutokana na mwanaume na mwanamke, na tumekujaalieni mapote na makabila mbalimbali ili mpate kufahamiana, hakika aliye mtukufu zaidi kati yenu kwa Mwenyezimungu ni huyo aliyemchamungu zadi katika nyinyi. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua, Mwenye khabari" (Al-Hujurat: 13)

**Inaendelea uk ..8**

# MAANGAMIZI YA GAZA NI MAANGAMIZI YETU SOTE UMMA WA KIISLAMU

Huu ni takriban mwaka wa pili tangu kijidola bandia cha Israel kilipoanza mashambulizi ya kikatili yanayoambatana na mauaji ya halaiki ndani ya Gaza kufuatia tukio la tarehe 7 Oktoba 2023.

Uvamizi wa kijidola cha mayahudi kwa agizo na nyenzo za kijeshi, kisiasa na kidiplomasia za Marekani na kuungwa mkono na nchi kadhaa za magharibi umeambatana na maangamizi yasiyo na mfano. Kuanzia mauaji makubwa ya halaiki kiasi cha kupotea roho za Waislamu 65,000 na majeruhi kwa maelfu, wengi wao wakiwa wanawake na watoto (kwa mujibu wa Wizara ya Afya ya Ukanda wa Gaza na vyombo vya habari vikubwa vya kimataifa). Ambapo vyanzo vingine vinaelezea hadi sasa zaidi ya watu laki mbili wameshauawa!

Aidha, uvamizi huo ambao umeshaangamiza takriban Gaza yote isipokuwa kijisehemu kidogo unachokimalizia kwa sasa, kando na kuvunjavunja takriban robo tatu ya majumba ya makaazi ya watu, umeleta uharibifu mkubwa sana kwa rasilmali watu na miundo mbinu mbalimbali. Kwa mfano, kuuwawa wanahabari zaidi ya 270, mpaka mwezi wa Agosti 2025 (Tv ya Al-Jazira), kuuwawa mamia ya walimu wakiwemo wa vyuo vikuu, kuuwawa wahudumu wa afya takriban 1400 (Relief web), kuvunjwa misikiti 79% (zaidi ya elfu moja), makanisa matatu ya Ukanda wa Gaza, kuuwawa




wanavyuoni wa Kiislamu zaidi ya 255 na wengine wengi kuwekwa kizuizini nk. (Wizara ya Waqfu- Gaza), Hospitali takriban 36 za Ukanda wa Gaza, zinazofanya kazi ni chache sana, nyingi zimevunjwa kwa mabomu nk. Bila ya kusahau uvamizi endelevu wa Israel kwa Ukanda wa Magharibi ukiambatana na mauaji, kuvunja majumba, kuharibu mashamba, kuwatoa watu katika majumba yao, kamatakamata kiholela nk.

Ukatili wote huo wa kijidola cha Israel na mauaji ya halaiki unajiri ilhali Marekani kwa mara ya sita inapiga kura ya turufu (veto) kuzuiya usitishaji wa uvamizi huo na mauaji hayo ya halaiki. Bila ya kutaja vitisho vya Marekani kwa Mahkama ya Kimataifa ya Jinai (ICC), kuitetea Israel licha ya Tume Huru ya Haki za binadamu ya Umoja wa Mataifa na baadhi ya taasisi za haki za binadamu za ndani ya Israil kutamka wazi hadharani kwamba dola ya Israil inatenda mauaji ya halaiki ndani ya Gaza.

**Enyi Majeshi katika Ulimwengu wa Nchi kubwa za Kiislamu hususan jirani na Israel,**

Munajua kwamba mna dhima mbele ya Mola wenu kuinusuru Gaza kwa kuwa mna nguvu mikononi mwenu? Jee mnajua kuwa nguvu mlizonazo ni amana kutoka kwa Mola wenu kwa ajili ya kunusuru Umma wenu na sio watawala vibaraka? Bado mna shaka juu ya uovu na ukatili wa kijidola bandia cha Israel? Mnasubiri nini kuikomboa Gaza? Bado munasitasita na muna imani na kijidola hicho pamoja na yote kinchoendelea kuyatenda ikiwemo Waziri wao mkuu kutangaza wazi lengo lao la kuzipora ardhi zetu kukamilisha mradi wao kufanya 'Israel kubwa' (Great Israel Project)

Au bado mna tamaa kwamba kijidola bandia cha Israel kitaleta amani, ilhali mnaona mbele ya macho yenu kila siku kinafanya mashambulizi Syria, Yemen, Lebaon, na hivi karibuni Qatar nk. Kijidola hicho hakiheshimu mamlaka ya nchi yoyote kwa mujibu wa sheria zao za kimataifa wala mikataba. Patilizeni fursa ya dhahabu kuimaliza Israel na kumuonesha Allah ujanadume wenu, ambao sisi hatuna shaka nao, na nyinyi ndio tumaini la Umma wetu.

**Enyi Wanazuoni vipenzi wa Kiislamu,**

Nani atawahesabu, kuwakosoa na kuwanyoosha watawala vibaraka katika ulimwengu wa Kiislamu ambao idhilali yao katika kuunga mkono Israeil imeruka mipaka ya aibu. Ndio watawala hawa vibaraka ambao hutumia bandari zao, anga zao,

**Inaendelea uk .. 8**

Maangamizi ya Gaza… Inatoka uk 7

rasilmali za Umma wa Kiislamu kukiwezesha kijidola cha Israel kuendelea kuiangamiza Gaza, halafu wakati huo huo eti wanaitaka Hamas iwaachie mateka na kusalimisha silaha zao. Ndio vibaraka hawa wanoaunga mkono sera ya hatari ya 'dola mbili' ambao ni mtego wa hatari wa kuipa Israil nguvu dhidi ya Umma wa Kiislamu. Mtego ambao baadhi ya nchi za magharibi kama Uingereza na Ufaransa wanajifanya kuunga mkono kama huruma kwa Waislamu wa Palestina, kumbe wanajificha nyuma yake, kwa kuwa tangu mwanzo wako bega kwa bega na Israil katika ukatili wake.

Pazeni sauti zenu Enyi Wanazuoni, tumieni mimbar zenu na majukwaa mengine kuwakosoa kwa ukali watawala vibaraka ambao wamefikia daraja duni hata kuliko watumwa. Jee hamuoni namna Qatar ilivyojipendekeza kwa Marekani kwa kumpatia Trump fedha na zawadi nyengine nono kisha Marekani inampa Israel silaha na ruhusa kuipiga nchi yake. Kuna aibu na fedheha kuliko hiyo? Trump na kijidola bandia cha Israil wanawachukulia watawala hawa ni vitimbakwiri duni kuliko hata paka. Enyi Wanazuoni hata muda ukirefuka vipi msiwaache mkono wala msiwachoke Waislamu wa Gaza, kwa kuwa wao ni Umma wetu. Basi changamsheni majeshi na changamsheni Umma usimame imara wasimime wajibu wao, na msiwasahau Waislamu wa Gaza kwa uchache walau dua katika misikiti yenu.

**Enyi Umma mtukufu wa Kiislamu,**

Mnajua kuwa ukimya wenu ni hatari kwa qadhia kama hii na mfano wake. Lau mtasimama kidete kwa sauti zenu mtawalazimisha wanavyuoni na wanajeshi nao kusimamia qadhia za Umma wenu. Basi msiingie katika mtego wa shetani wa kunyamaza kimya.

Jee mnashindwa na makafiri wanapaza sauti zao kutetea Gaza kwa kusukumwa na ubinadamu tu, ilhali nyinyi mna imani na udugu wa Kiislamu. Sauti zenu ni wajibu ili kuwahimiza wanavyuoni na wanajeshi wa nchi kubwa za Kiislamu kuchukua hatua.

Kwa kumalizia, yanayoendelea Gaza na madhila mengine katika ulimwengu wa Kiislamu ni matokeo ya Umma wetu kukosa dola ya Khilafah kulinda na kusimamia mambo ya Umma wetu ikiwemo kuhifadhi mali, heshima na damu zetu. Ni wajibu kujifunga na ufaradhi wa ulinganizi wa kurejesha tena dola yetu ambayo ndio kinga ya kweli ya kila chetu.

*********************

Siku ya afya… kutoka uk 6

Ufahamu huo humfanya mwanadamu kutojidharau yeye mwenyewe kwa kujilinganisha kipato, elimu, muonekano na wengine bali kipimo chake cha ubora au thamani ni uchamungu na kwa kujipima huku kutamfanya azidi kumcha Mola wake maishani pasi na kujali lawama za wenye kulaumu wala kashfa za wenye kukashfu.

Uislamu pia ukaja ukatibu tatizo la msongo wa mawazo ambao hupelekea sonona (depression) kwa kumpa mtazamo thabiti juu ya maisha ya dunia, tafsiri yake juu ya mafanikio ya kweli ya mwanadamu na kipimo sahihi cha thamani ya mwanadamu.
Aidha, Uislamu ukamuondolea mwanadamu wasiwasi juu ya suala la rizki, kuwa Allah (s.w) ndio Mpaji wa rizki na hakuna atakaekufa isipokua ametimiliza rizki yake.

Pia Uislamu ukamjenga Muislamu juu katika fikra ya subra katika mitihani na kutokukata tama na rehma za Mola wake.

Haya katika upande wa kifikra na nidhamu za kivitendo katika uchumi, jamii nk yatosha kabisa kumzuiya mwanadamu kupata misongo ya mwazo isiyo ya lazima na kumpa utulivu na amani ya nafsi itakayomfanya kuishi kwa furaha licha ya kuwa mnyonge au dhaifu katika upande wa kimadania.

Dr. Abdul-Malik
Shamsudin

*************

USIKOSE KUSOMA JARIDA
LAKO LA KHLAFAH
KILA MWEZI